



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA



TANGAZO LA NAFASI YA KAZI MAALUM YA KUKUSANYA USHURU KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga anapenda kuwatangaza nafasi za kazi maalum kwa watazania wenye sifa kama ifuatavyo:-

MKUSANYA USHURU – NAFASI 31

SIFA :

- Mwombaji lazima awe Raia wa Tanzania.
- Awe na elimu ya Kidato cha Nne,
- Awe mwaminifu

KAZI NA MAJUKUMU:

- i. Kukusanya mapato kutoka katika vyanzo vya Halmashauri.
- ii. Kutunza kumbukumbu za hesabu.
- iii. Kupeleka fedha alizokusanya benki kila siku.
- iv. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa Kazi

MASHARTI YA JUMLA:

- Awe amehitimu na kupata Cheti cha Taaluma cha Kidato cha Nne (IV)
- Awe na Cheti cha Kuzaliwa.
- Barua zote za maombi ziambatane na nyaraka zifuatazo:-
 - i. Nakala za Vyeti vya mwombaji vilivyothibitishwa.
 - ii. Maelekezo binafsi ya mwombaji (Curriculum Vitae).
 - iii. Barua ya Mdhamini.
 - iv. Picha ndogo za rangi (Coloured Passport Size) mbili (2) za Mwombaji za hivi Karibuni.
- Kila mwombaji lazima awe na Umri kati ya miaka **18 - 45**.
- Barua ambazo hazikuambatishwa na nyaraka zilizotajwa hapo juu (i – iv) hazitafanyiwa kazi.


JINSI YA KUTUMA MAOMBI:

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono, zikiwa na anwani kamili ya Mwombaji, pamoja na namba ya simu na zitumwe kwa anuani ifuatayo:-

**MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
S.L.P. 19
IGUNGA.**

TAREHE YA MWISHO YA KUPOKEA MAOMBI:

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **09/09/2021** saa **9.30** Alasiri


Fatuma O. Latu
**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
IGUNGA**
**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA IGUNGA**